

# Uwawa - Ushirikiano wa Wazazi na Walimu

## MPANGO MZIMA



Na Cecilia Dembe- Kibiti DC

**Wakuu wa shule, waratibu Elimu kata, na Wenyeviti wa kamati za shule za msingi Wilayani Kibiti wamepatiwa mafunzo ya uundaji wa kamati za Ushirikiano wa Wazazi na Walimu-(Uwawa).**

**Mafunzo hayo ya siku tatu yanayoratibiwa na Programu ya Shule bora, inayo jikita katika uboreshaji wa Elimu ya awali na Msingi kwa ufadhilli wa Shirika la Msaada la uingereza UK aid kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania yameanza leo Mach 18 na yanatarajiwa kuisha Machi 20/2023**



**Donatus Mlelwa**

**“ Wazazi na Walimu wanajukumu Kubwa la kuhakikisha usalama wa watoto wawapo shulenii au nyumbani ”**

### **Washiriki wa Mafunzo hayo wakibainisha matarajio yao baada ya mafunzo hayo**



**Mhe. Omary Twanga**

Akizungumza katika uzinduzi wa mafunzo hayo Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibiti Mhe. Omary Twanga amesema kuwa mafunzo hayo adhimu yatabadilisha kabisa hali ya shule nyingi hususani katika taaluma za watoto wetu endapo tuu yatiliwa mkazo kama ambavyo serikali imepanga kuitia mradi wa Shule bora.



**washiriki wa mafunzo hayo wamebaini kuwa ushiriki wa Wazazi katika masuala yote yanayohusu taaluma ya mwanafunzi ni muhimu mno, Hivyo wazazi wanawajibu wa kubaini na kuwashirikisha walimu changamoto zinazohusu ustawi, usalama na ujumuishi wa wanafunzi ili kujenga taaluma bora kwa watoto wetu.**



**Aidha washiriki wa mafunzo hayo wameahidi kwenda kutekeleza kwa weledi yote waliyojifunza mara tuu baada ya kumaliza mafunzo hayo**

Naye mtaalamu wa Afua (intervention specialist) ndg. Donatus Mlelwa amewaeleza washiriki wa mafunzo hayo kuwa wazazi wakishirikishwa ipasavyo watasaidia kuimarishta ustawi na usalama wa watoto kwani utafiti usio rasmi unaonyesha kuwa wazazi wamekuwa mbali na watoto kimalezi hivyo watoto wanakosa mtu wa karibu wa kumweleza changamoto zinazowasibu hatimaye kufikia hatua ya kufanyiwa vitendo vya kikatili na udhalilishaji.